ISSUE 001
22.02.2024



# Mfumo wa Kitaifa wa Upangaji wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari (MSP), Kenya

## NAKALA YA MAELEZO KAMILI

Mfumo huu wa kitaifa unaelezea njia ambayo inafuatwa na nchi ya Kenya katika kuandaa Upangaji wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari (MSP) na utatumika kama mwongozo wa kimsingi wa mchakato wa MSP humu nchini na katika sekta za uchumi samawati. Nakala hii ya maelezo kamili inaeleza vipengele muhimu vilivyoshughulikiwa katika mfumo huu.



## Mchakato utaegemezwa wapi?

Mfumo huu unazingatia uhusiano na mipango ya maendeleo ya kitaifa, mipango jumuishi ya maendeleo ya kaunti (CIDP), ajenda za kikanda na kimataifa. Haya ni pamoja na; ruwaza ya Kenya 2030, Mpango wa IV wa awamu ya Kati na Ajenda ya Mageuzi ya Kiuchumi ya kufaidisha watu wa chini kueleka juu. (BETA).

Mfumo huu pia unaongoza ujumuishaji wa MSP katika CIDPs na Mipango ya Maeneo ya Kaunti (CSPs). Inawiana na Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063, Ajenda ya 2050 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Mkataba wa Nairobi na ajenda ya Jumuiya ya Sayansi ya Magharibi ya Bahari Hindi (WIOMSA).

## Mchakato wa Maandalizi

Mfumo wa MSP unaeleza na kunakili awamu za maandalizi ya mipango. Unatoa mpangokazi wa kila hatua na vipengele vinavyohusiana kama vile Tathmini ya Kimkakati na ya Kijamii ya Mazingira (SESA),na ukusanyaji wa data na uchambuzi.

## Umuhimu wa Mfumo wa MSP

- Kutoa matarajio ya kiwango cha kitaifa kwa ajili ya mipango ya matumizi ya sasa na ya baadaye ya maeneo ya bahari
- Kupangilia mchakato na maendeleo ya kitaifa, vipaumbele, mifumo ya maendeleo ya kikanda na kimataifa
- Kueleza mchakato wa upangaji wa matumizi ya maeneo ya baharini na utekelezaji wake
- Kutoa kanuni muhimu na vipengele vinavyoongoza mchakato wa MSP nchini Kenya.



## Muktadha wa Kisheria na Kitaasisi

Mfumo umeimarisha miundo ifuatayo inayohusika katika mchakato wa maandalizi ya MSP;

- Kamati Tendaji
- Kamati ya Uendeshaji wa Wakala Mbalimbali wa MSP (MSP-MASC)
- Sekretarieti ya MSP
- Vikundi vya Kazi ya Ufundi vya MSP.

## Uwezo wa Wahusika wa Kutekeleza MSP

Mfumo huu unashughulikia yafuatayo;

- Unabainisha ujuzi na utaalamu unaohitajika katika maandalizi na utekelezaji wa MSP
- Unatambua mafunzo muhimu yanayohitajika ili kutekeleza mpango huo
- Unachunguza uhamishaji wa maarifa kutoka nchi zilizotekeleza mipango kama hiyo
- Unachukua mbinu bora za kimataifa na kuongozwa na utafiti wa kisayansi.

## Mifumo ya Ufadhili

MSP inafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Kenya. Hata hivyo, inatarajiwa kuwa mifumo tofauti ya ufadhili, kama vile ushirikiano kati ya umma na mashirika ya kibinafsi na dhamana, itajumuishwa ili kuhakikisha mchakato huo unadumu.

## Ushirikishaji wa Wadau

Mfumo unatambua kuwa maandalizi ya MSP ni mchakato wa umma na kisiasa. Kwa hivyo, umeingiza uchambuzi wa kina wa wadau ili kutoa mkakati wa kina ambao unahakikisha wadau wote wanahusishwa, maslahi na matarajio yao yanashughulikiwa, na majukumu yao yanaelezwa wazi.

## Mawasiliano kwa MSP

Mfumo unaanzisha mkakati wa mawasiliano ili kuhakikisha wadau wanapata taarifa sahihi kuhusu mchakato wa MSP na kuhamasishwa kushiriki katika hatua mbalimbali za maandalizi, maendeleo na utekelezaji. Hii itafanikiwa kupitia uwasilishaji wa nyenzo za mawasiliano, vikao vya mazungumzo na kubadilishana mawazo na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu MSP.

## Kudhibiti Hatari

Mfumo wa kina wa kudhibiti hatari utaandaliwa na mikakati ya kupunguza athari kukubaliwa. Mikakati hii inajumuisha utekelezaji wa mifumo ya ulinzi, ushirikishaji wa wadau, mkakati wa mawasiliano na muundo wa matumizi ya fedha katika awamu ya kati.

## Ufuatiliaji na Utekelezaji

Mpango Mbinu zitakazotumika ili kuhakikisha mipango inatekelezwa vyema zitawekwa. Hatua zitachukuliwa kwa wale ambao hawazingatii mipango na motisha zitatolewa kwa sekta zinazotekeleza na kufuata mipango..

## Kupima Maendeleo

Mpango wa ufuatiliaji na tathmini wenye viashiria muhimu vya utendaji utawekwa ili kufuatilia maendeleo dhidi ya malengo. Hii itasaidia kuboresha mara kwa mara kwa ufanisi ili kufikia matokeo.




Madhumuni ya mpango Mpango  wa Taifa wa Matumizi ya Maeneo ya Baharini  ni kuandaa mfumo wa haya maeneo kwa ujumuishaji na uratibu wa sera za kijamii na kitamaduni, mazingira na kiuchumi kwa maendeleo ya kasi ya uchumi utokanao na raslimali za majini.

The National Project Coordinator
KEMFSED
Maktaba Kuu Building, Ngong Road, Upper Hill, Mezzanine Floor
Tel : +2540207860430
MSP Secretariat email: complaints@msp.go.ke
Website: https://msp.go.ke/

Utayarishaji wa nakala hii umefanikishwa na mradi wa KEMFSED kupitia ufadhili wa Serikali ya Kenya na Benki ya Dunia.